

MTIHANI WA PAMOJA WA SHULE ZA MKOA WILAYANI THIKA 2009

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 3

LUGHA

JULAI / AGOSTI 2009

SAA: 2 ½

Maagizo

- Jibu maswali manne pekee.
- Swali la kwanza ni la lazima
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani;
- Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi ushairi.
- Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

FASIHI SIMULIZI

1. (a) Tofauti misemo, nahau, misimu na lakabu. (alama 4)
(b) Fafanua umuhimu wa misimu kama kiperi cha fasihi simulizi (alama 8)
(c) Eleza sifa za malumbano ya utani. (alama 4)
(d) Eleza sifa za nyimbo za siasa. (alama 4)

TAMTHILIA

Kithaka wa Mberia: Kifo Kisimani.

2. Taja na ueleze aina za migogoro inayojitokeza katika tamthilia ya kifo kisimani (alama 20)

RIWAYA

Said A Mohamed: utengano.

Jibu swali la 3 au 4.

3. Haloo, nani? Aha Mr. Smith..... ni wewe. Nilikuwa nakusubiri kwa hamu. NdiyoNitafanya kama ulivyoagiza.

- (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

- (b) Kabla ya mazungumzo haya kujiri, kulikuwa na ushairi wa “ kilio cha Mnyonge”. Taja ujumbe unaojitokeza katika ushairi huu. (alama 6)
- (c) Mzungumzaji katika muktadha huu alikuwa mwovu. Thibitisha. (10 marks)

Au

4. Mwiba wa kujichoma hauna kilio. Thibitisha kwa kuzingatia wahusika watano katika riwaya ya Utengano. (20 marks)

HADITHI FUPI

K.W. WAMITILA: MAYAI WAZIRI WA MARADHI

Jibu swali la 5 au la 6.

5. Diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi imejikita katika masuala ibuka yayayofaa kushughulikiwa na jamii. Taja na uthibitisha. (alama 20)
6. ‘sote tulisimama ghafla kama tumesimikwa ardhini. Woga ulituingia na kutukausha miili yetu. “Huu mwisho wetu sasa!”
- (a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
- (b) Taja mbinu tatu za lugha zilizotumika katika dondoo hili. (alama 3)
- (c) “Nilikumbuka ile sura ya mama na ndugu zangu.” Ni kwa nini msemaji anawakumbuka mama na ndugu zake? (alama 4)
- (d) eleza maudhui yanayoibuka katika muktadha huu. (alama 6)
- (e) Taja matatizo matatu yaliyowakabili wakimbizi. (alama 3)

USHAIRI:

7. soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuata.

- | | |
|--|--|
| 1. Ni sumu, sumu hatari.
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako leweshi
Za kupanda ngazi,
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa wazazi | 2 Ni sumu, sumu hasiri
Unahasiri watoto
kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika,
pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi.
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi |
| 3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi | 4. Ni sumu, jeruhi
Unajeruhi watoto kwa pesa,
kwa mapenzi yako hatari |

Ya daima kunywa ‘moja baridi’
Yanakufunga katika kiabu
Hadi saa nane usiku
Huku yakijenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi.

Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa,
Na kasha kwenye madawa ya kulevya
Barabara inayofikisha kwenye giza baridi
La karibu la asubuhi

(Kutoka: bara Jingine, K. wa Mberia Marimba, uk48-49)

MASWALI

- (a) Pendekeza kichwa kwa shairi hili. (alama 1)
- (b) Fafanua maudhui ya shairi hili. (alama 4)
- (c) Ni kwa njia gani kinachozungumziwa kinajenga ukuta? (alama 2)
- (d) Dondoa tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi na uzitolee mifano.
- (e) Eleza umbo la shairi hili (alama 3)
- (f) Uandike ubeti wa nne kwa lugha nathari. (alama 4)
- (g) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi.
 - (i) Giza baridi
 - (ii) yanakufunga katika Kiabu.